# MPOKEE YESU

## UUINGIE UFALME WA MBINGUNI

(Maombi ya Ukombozi & Damu ya Yesu)

✞

Karibu sana katika ufalme wa Mbinguni wa **Yesu Kristowa Nazareti** ambaye ni Mfalme na Mungu anayeishi. Yesu Kristo ndiye njia pekee na kweli ya kwenda Mbinguni **(Yohana 14: 6).**

Acha maisha ya dhambi, mrudie Bwana sasa, kanisa Takatifu la Bwana linakaribia nyakuliwa.Uingie ufalme wa Mbinguni kabla haujaondolewa.Tumenunuliwa kwa thamani na gharama pale **Kalvari**, tumerudishiwa uwezo,nguvu na mamlaka tena kupitia **Kristo Yesu** ( ***Nguvu ya Msalaba na Damu ya Yesu***) iliyomwagika pale **Kalvari, (1Wakorintho 6:19-20).** Damu ya Yesu imetupa uwezo wa kushinda vita na kutuweka huru, mbali na mateso na vifungo vya shetani.Kwa sasa shetani hana nguvu wala mamlaka tena juu yetu, tumepewa mamlaka ya kumshinda kwa Damu ya Mwokozi wetu Yesu Kristo (**Damu ya Mwana Kondoo**). **Ufunuo wa Yohana 12:11.**

**Mpe Yesu** maisha yako sasa ayamiliki na uuingie Ufalme wake wa Mbinguni, chagua Nuru na ukubali kuishi maisha matakatifu. Yesu ndiye njia pekee ,hakuna atayeiona Mbingu wala kuuingia Ufalme wa Mbinguni pasipo kumkili Yesu kuwa Bwana na mwokozi wa maisha yake.

Nakubariki kwa Jina la Yesu Kristo ambaye ni Bwana na Mwokozi wa maisha yetu amina.

**Mungu akubariki,**
**Petrida Karch.**

# YALIYOMO

Ufalme wa Mbinguni Duniani......................................4

Sala ya Kumpokea Yesu................................................6

Sheria za Ufalme wa Mbinguni.....................................7

Faida za kuokoa/mpokea Yesu.......................................8

Agano la Damu ya Yesu na Nguvu ya Msalaba kwa Wanadamu.........................................................................11

Nguvu ya Damu ya Yesu kwa Wanadamu .....................13

Nguvu ya Msalaba wa Yesu kwa Wanadamu… ..............14

Maombi ya kufunguliwa vifungo na magonjwa mbalimbali… ....................................................................... 16

Ujumbe wangu kwako............................................................20

## UFALME WA MBINGUNI DUNIANI

Ulimwengu huu uliumbwa uwe mwendelezo wa ufalme wa Mbinguni lakini katika mfumo wa kimwili.Mungu ni Neno kupitia Neno lake aliumba Mbingu na dunia na hii ndiyo sababu kubwa inayotufanya kutambua kuwa Neno la Mungu ni Mungu mwenyewe.Mbingu ni ya Mungu,dunia aliwapa wanadamu ndiyo maana kupitia Neno lake alimwumba mwanadamu (Adamu na Hawa) ili Mungu apate kumiliki,tawala na tiisha dunia kupitiawanadamu kama roho iishiyo ndani yao**. Mathayo 25:34.**Wanadamu wamepewa jukumu la kumiliki, tawala na tiisha dunia kama wana wa Mungu **(Watoto wa Mungu). (Mwanzo 1:26-27, Zaburi 115:16).**

Dhambi ilimfanya mwanadamu apoteze uwezo wake na mamlaka ya kumiliki na kutawala dunia.Dhambi ilisababisha mapinduzi ya serikali ya Mungu wa Mbinguni hapa duniani na kuingizwa serikali ingine ya giza katika utawala.Mwanadamu wa kwanza aliishi katika bustani ya Edeni ambayo katika ulimwengu wa roho ni kama ufalme wa Mbinguni hapa duniani na baada ya kutenda dhambi ya kula tunda la katikati walitenda dhambi ambayo iliwafarakanisha na Mungu na mahusiano yao yalivunjika. Dhambi ilisababisha uasi,ambao ni usaliti, au kwenda kinyume na taratibu za kisheria.Dhambi ilivunja agano kati ya Mungu na wanadamu (Agano la kuitwa wana wa Mungu na wana wa ufalme).

Toba/msamaha uliweza rudisha tena ufalme huu wa Mbinguni duniani na haki zake zote kama mwanzo tulizopewa na Mungu kupitia Yesu Kristo. Hii ndiyo sababu Mungu kwa upendo wake kuamua kumtuma mwana wake wa pekee kuja duniani iliapate komboa ulimwengu kwa damu yake.**Ufunuo wa Yohana 5:9-10.** Ufalme wa Mbinguni umesharudi duniani kupitia Yesu Kristo kama Mfalme wetu na Yehova kama Mungu wetu **(Mungu wa Mbinguni anayeishi**).Njia pekee ya kuurudisha ufalme huu ni kwa njia ya toba **(msamaha au kuokoka), Mathayo 4:17.**

***Tangu wakati huo, Yesu alianza kuhubiri akisema: "Tubuni, kwa maana Ufalme wa mbinguni umekaribia."***

Yesu ndiye njia ya kweli na uzima. Huwezi uingia Ufalme wa Mbinguni pasipo kumkiri Yesu Kristo kuwa Bwana na mwokozi wa maisha yako.
Sali sala hii Pamoja nami kwa sauti ili upate mpokea Yesu Kristo wa Nazareti na kuuingia Ufalme wake wa Mbinguni (Ufalme wa milele).

## SALA YA KUMPOKEA YESU - KUOKOKA

Baba katika jina la Yesu Kristo wa Nazareti aliye hai, Bwana Yesu ninaomba msamaha kwa dhambi zangu zote nilizotenda tangu utoto wangu hadi sasa. Ninaomba ulifute jina langu katika kitabu cha kuzimu na mauti na uliandike jina langu katika kitabu cha uzima wa milele.Ninamkana shetani na mamlaka zake zote za giza. Ninakukiri wewe Yesu Kristo wa Nazareti na ninakupokea leo wewe Bwana,uwe Bwana na mwokozi wa maisha yangu yote. Miliki maisha yangu,nafsi yangu na roho yangu pia. Ahsante Bwana Yesu kwa kunikomboa,kunisamehe dhambi zangu na kuniweka huru **Amina.**

Iwapo umesali sala hii kwa Imani, tambua kuwa umeokoka na Yesu Kristo anaishi ndani yako (moyoni mwako). Karibu sana katika ufalme wa Mbinguni (Mungu anayeishi). Kwa kumpokea Yesu umejenga uhusiano mzuri kati yako na Yesu kristo na Mungu wa Mbinguni maana kwa sala hii umepokea vitu vitatu ;

**1.Yesu Kristo.**
**2.Roho Mtakatifu.**
**3. Umekuwa mwana wa Mungu aliye hai na wewe pia ni hai.**

Usimwache Yesu endelea na wokovu, tunza vazi lako la utakatifu Kanisa la Bwana li karibu nyakuliwa,usikose Mbingu.

✞

# SHERIA ZA UFALME WA MBINGUNI

Kila Ufalme una Mfalme, sheria na ulinzi unaolinda ufalme huo. Ufalme wa Mbinguni Mfalme wake ni **Yesu Kristo,Mungu wake ni Yehova**, sheria zake zimebebwa na **Biblia takatifu** na ulinzi wake unalindwa na askari waitwao **Malaika watakatifu.**Ufalme huu unaongozwa katika ulimwengu wa roho (ulimwengu usioonekana kwa macho ya nyama). Ufalme huu unaongozwa kwa njia ya **Imani** na njia pekee ya mawasiliano kati ya Mungu na watu wake ni **maombi(sala),maono,ndoto,Neno la Mungu,mahubili toka kwa watumishi wake wa kweli.**Mtu ni watu wawili katika mmoja.Watu hawa wanaishi pamoja na watatenganishwa na **kifo** tu.Yupo mtu wa ndani na nje. Mtu wa nje ni **mwili wako** wa nje na ndani ni **nafsi yako** itayoishi milele.Mtu wa ndani ameumbwa na **roho pamoja na nafsi.** Hivyo nafsi imebeba roho,unapokufa roho iliyobebwa na nafsi inauacha mwili wako wa nje na unaenda Mbinguni au kuzimu kwa ajili ya kusubili hukumu ya mwisho.

Ulimwengu wa roho umegawanyika makundi mawili;

- **Ulimwengu wa Nuru (Ufalmewa Mbinguni).**
- **Ufalme wa giza (Ufalme washetani).**

Neno la Mungu ni Mungu mwenyewe, Neno la Mungu ni kinga au ngao kati ya watu wa Mungu na shetani. Sheria za Ufalme huu ni matendo mema na yale yaliyoandikwa katika **Torati na Musa (Kumbukumbu la Torati 5: 6 – 22).**

Mtu wa ndani anakuzwa /anaishi kwa **Neno** kusoma Biblia,kusali,kusikiliza mahubiri ya watumishi wa kweli,kufunga nakutenda matendo mema.

**Mathayo 4:4**
***"Yesu akamjibu, "Imeandikwa: 'Mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu".***

Shika sana Neno la Mungu, usimwache Yesu yu karibu kuja kwa kanisa lake Takatifu.Unabii umeshatimia mengi yaliyotabiriwa yameshatimia.Unabii wa **Ufunuo wa Yohana na Daniel** ushatokea na kutimia ,Mfalme wetu yu karibu kuja kwa unyakuo wa kanisa lake Takatifu.Acha dhambi mrudie Bwana, lango la wokovu na rehema bado lipo wazi,li karibu kufungwa na unyakuo kutokea.

## FAIDA ZA KUOKOKA (UFALME WA MBINGUNI)

Watu wengi hawajui faida na umuhimu wa kumpokea Yesu. Hakuna faida kubwa duniani kama kuwa na Yesu ndani yako na kuuishi ufalme huu wa sasa na milele. Yesu ndiye njia au lango pekee la kuingia ufalme huu wa Mungu anayeishi **(Yohana 14: 6).** Mlango huu unauingia pale tu unapompokea Yesu Kristo kuwa Bwana na mwokozi wa Maisha yako.

***Faida za kuokoka/Kumpokea Yesu.***

**1.** Jina lako linaandikwa katika kitabu cha uzima wa milele Mbinguni.

**2.** Hakuna magonjwa katika ufalme huu bali uzima wa milele.

**3.** Umepokea uzima wa milele kwa sasa na maisha ya baadae baada ya kifo (baada ya hukumu.

**4.** Unalindwa na Malaika watakatifu muda wote hapa duniani.

**5.** Hulogwi wala huonewi na nguvu za giza **(Hesabu 23:23).**

**6.** Umehama ulimwengu wa giza na umehamia ulimwengu wa nuru unaoongozwa na Yesu Kristo kama Mfalme na Yehova kama Mungu wa ufalme huu.

**7.** Umesamehewa dhambi, laana imefutika juu yako na sasa u hai na umepokea baraka kupitia Yesu Kristo. **(Isaya 43:25 na Isaya1:18).**

**8.** Umepokea ulinzi toka ufalme huu wa Nuru, unalindwa maisha yako yote muda wote.

**9.** Utapata tambua/ona ya jayo kabla ya wengine **(Maisha yako ya jayo)**kwa nguvu ya Roho Mtakatifu uliyepewa baada ya kuokoka.

Napenda kukutia moyo zaidi, umechagua njia sahihi,umechagua baraka na uhakika wa maisha yako ya sasa na yajayo.Umemchagua Yesu na umemkataa shetani,umechagua kwenda Mbinguni na umekataa kwenda motoni **(Ufunuo wa Yohana 20:15).**

## Nini kimetokea baada ya kuokoka/kumpokea Yesu katika maisha yako?

Baada ya kuokoka wewe ni kiumbe kipya, umezaliwa mara ya pili katika ulimwengu wa roho.Kwa kumpokea Yesu umechagua maisha mapya, maisha **ya baraka na amani** maana **Yesu** ni baraka na amani.**(Yakobo 3:10).** Uliposali sala ya kumpokea Yesu ulitumia kinywa,hivyo ulichagua baraka ambayo ni Yesu mwenyewe na ulikana laana.

Hongera sana kwa hilo.Wote wasiompokea Yesu (wasiookoka) wanaishi chini ya laana ya Mungu aliyoiachia duniani baada ya dhambi kuingia ulimwenguni kupitia **Adamu na Hawa.** Kupitia **Damu ya Yesu** tumeweza futiwa laana hii na kuwa huru toka mateka ya shetani yaliyo chini ya laana. Faida zingine utazopata baada ya kumpokea Yesu maishani mwako;

1) **1.**Umesamehewa dhambi zako zote **(1Yohana 1:9).**

2) Jina lako limeandikwa katika kitabu cha uzima wa milele Mbinguni **(Luka 10:20).**

3) Umekuwa kiumbe kipya **(2 Wakorintho 5:17 na Waefeso 4:22-24)**

4) Unalindwa na Malaika watakatifu muda wote **(Zaburi 91:11-12).**

5) Umekuwa makao makuu ya Kristo na Mungu hapa duniani **(Yohana 14:23 na Waefeso 2:22).**

6) Roho Mtakatifu anaishi ndani yako **(1Wakorintho 6:19).**

7) Ulipokea mamlaka juu ya shetani na wakala wake na kazi zao zote hazina nguvu kwako (**Luka 10:19 na Yakobo 4:7).**

8) Utafufuliwa na kunyakuliwa na Yesu akija chukua kanisa lake(waliookoka) maana unao uzima wa milele. **(1 Wathesalonike 4:16-17 na 1 Yohana 5:12)**

✞

# AGANO LA DAMU YA YESU NA NGUVU YA MSALABA KWA WANADAMU



Damu ya Yesu imebeba agano kwa wanadamu, ina uwezo wa kumshinda shetani na ufalme wake hasa katika siku hizi za mwisho kabla ya unyakuo***(Ufunuo wa Yohana 12.11).*** Tumenunuliwa kwa Damu ya thamani ya mwokozi wetu **Yesu Kristo wa Nazareti** tumekuwa huru si watumwa wa dhambi tena **(1Wakorintho 6:19-20).**Ingawa shetani ni mungu wa dunia hii tumepewa mamlaka ya kumshinda kupitia **Damu ya mwana Kondoo (Damu ya Yesu - Ufunuo wa Yohana 12:11)**. Kuanzia sasa shetani hana nguvu tena kwetu tumepewa uwezo, nguvu na Mamlaka kupitia **Kristo Yesu** (Nguvu ya Msalaba na Damu ya mwokozi wetu **Yesu Kristo**) iliyomwagika pale **Kalvari** kutushindia vita na kutuweka huru, mbali na mateso na vifungo vya shetani.

Ulimwengu unapitia nyakati za mwisho, kipindi tunachojiandaa kwa unyakuo wa kanisa **(Kurudi kwa Bwana wetu na mwokozi wetu Yesu Kristo wa Nazareti)** kwa kanisa lake Takatifu. Kipindi hiki si chepesi kwa dunia kutokana na vita vya **kiiman**i vinavyozuia wengi wasiingie **Ufalme wa Mbinguni na kuishia jehanamu (motoni). Jina la Yesu, Roho Mtakatifu, Neno la Mungu na Nguvu ya Msalaba** vyote vinanguvu ila **Damu ya Yesu** inanguvu zaidi kwa kipindi hiki cha maandalizi ya unyakuo wa kanisa. **Ufunuo wa Yohana** ni kitabu kinachoeleza nyakati za mwisho dunia tunachopitia kabla ya unyakuo, baada ya unyakuo na kufutwa kwa dunia. **Ufalme wa giza (shetani)**

**anatumia nguvu kubwa kuzuia wanadamu wengi wasimrudie Mungu anayeishi,kukosa unyakuo na kutopokea wokovu**. Tunapitia vita vya kiroho ambavyo kwa nguvu zetu za kibinadamu hatuwezi mshinda shetani isipokuwa kwa nguvu ya **Roho Mtakatifu na Damu ya Yesu** ambayo imefanya Agano nasi hasa katika nyakati hizi za mwisho **Ufunuo wa Yohana 12:11.**

***"Nao wakamshinda kwa damu ya Mwana-Kondoo, na kwa neno la ushuhuda wao,ambao hawakupenda maisha yao hata kufa"***

## MAENEO SITA DAMU YA YESU ILIPOTOKA

1. **Damu usoni** - Yesu alipokuwa akisali **Mlimani Gethsemane Luka 22:41 – 44** Damu hii ilitoka wakati Yesu akiomba, matone ya Damu toka usoni mwake.Wanadamu tulipokea Kibali cha uso,nyota,utiishi wa Mungu ndani yetu na kufungua vifungo vyote **vinavyohusu vibali tulivyofungwa na Ibilisi (Shetani).**

2. **Damu ya Mgongoni** – Yesu alipopigwa mijeredi mgongoni Damu hii ilitumika katika **utabibu na kutuweka huru na magonjwa yote.**

3. **Damu mikononi** – Yesu alipogongelewa misumali mikononi Damu yake ilitupa mamlaka ya kuponya,kuweka mikono juu ya wagonjwa na kupokea uponyaji.Tulipokea kibali cha kuponya magonjwa yote, **Marko 16:17 -18.**

4. **Damu miguuni** – Damu ya Yesu iliyomwagika miguuni baada ya kugongelewa msumali ilitupa uhalali wa kumiliki,kutiisha na kushinda nguvu zote za yule adui. **Zaburi 91:13, Luka 10:19, Zaburi 60:12.**

5. **Damu Kichwani** – Yesu alipovishwa taji la miiba,Damu yake ilifuta laana zote wanadamu tulizolaaniwa kupitia ardhi na shetani na kufungua ufahamu,fikra na akili zetu

wanadamu na kutuweka huru, **Mwanzo 3:17-18).**

6. **Damu Ubavuni** – Damu ya Yesu iliyomwagika ubavuni baada ya askari kumchoma Yesu mkuki ubavuni kuhakikisha kama amekufa.Damu na maji yalimwagika,**maji ni maji ya uzima wanadamu tulipokea uzima wa milele** na Damu yake ilishinda **nguvu ya mauti na kuturudishia uhai tena duniani. Yohana 19:33-34, Zaburi 118:17).**

**NGUVU YA DAMU YA YESU KWA WANADAMU**

Shetani anaogopa sana Damu ya Yesu ndo maana hapendi Damu ya Yesu itumike kwa kuwa imebeba **Agano kwa wanadamu** na ina nguvu ya kumshinda hasa katika nyakati hizi za mwisho.

1. **Damu ya Yesu** -imebeba uhai imefuta ufu na kutupatia uhai tena.Kupitia uhai tuliopokea imetuunganisha na Mungu kwa njia ya upatanisho,**Warumi 3:25**.
2. **Damu ya Yesu**-Imetufanya kuwa mali ya Mungu,Damu hii imetununua mikononi mwa adui na kutufanya kuwa huru.Tumekuwa mali ya Mungu anayeishi hatumilikiwi tena na shetani.Tumenunuliwa kwa Damu ya thamani na sasa tupo huru, **Ufunuo wa Yohana 5:9, Matendo ya Mitume 20:28, 1 Petro 1:18-19.**
3. **Damu ya Yesu -Imefuta** dhambi zetu na kutufanya kuwa huru na wapya,**Mathayo 26:27-28, Waebrania 9:22, 1Yohana1:7.**
4. **Damu ya Yesu** - Inatupa ulinzi duniani, inatufunika na kutulinda na nguvu za giza,magonjwa yote na mashambulizi yote ya adui (shetani).
5. **Damu ya Yesu** – Inatupa ujasiri wa kushindana,kushinda vita vya kiroho tunavyopigana na shetani na hata kuweza karibia kiti cha enzi cha Mbinguni kwa kuwa imetusafisha na kutupa kibali mbele za Mungu,**Waebrania 10:19**.

## WIMBO

*Damu ya Yesu* × 3
*Husafisha kabisa,*
*Na nguvu za shetani zimeshindwa na Yesu* × 3
*Asifiwe mwokozi*
*Na nguvu za mapepo zimeshindwa na Yesu* × 3
*Asifiwe mwokozi.*
*Siku moja Yesu,atarudi* × 3
*Kuchukua kanisa.*

## NGUVU YA MSALABA KWA WANADAMU

Imo nguvu ndani ya Msalaba,Kwa kupigwa kwake Yesu tumekuwa huru.Nguvu ya Msalaba imetuweka huru nafsi zetu toka ufu na mauti na kupokea uzima wa milele.Tunaishi pamoja na Yesu Kristo kupitia nguvu ya msalaba tuliyopokea pale msalabani.Kila amwaniniye Yesu ameusurubisha mwili wake toka mautini na kupokea uzima wa milele pamoja na Yesu.Tulikuwa wafu kupitia dhambi na sasa tunaishi pamoja na Yesu.

1. **Nguvu ya Msalaba** -imetukomboa nafsi zetu.Nafsi ni mtu wako wa ndani anayeishi milele aliyebeba roho ndani yake ambaye Yesu amemnunua pale msalabani na kumweka huru na hukumu ya Jehanamu na kuuingia uzima wa milele(Ufalme wa Mbinguni) wa Mungu anayeishi.
2. **Nguvu ya msalaba**-Imetuamisha toka ufalme wa giza na kutuingiza ufalme wa Nuru wa Mwana Kondoo (Yesu Kristo wa Nazareti).Imetufanya kuwa mali na milki ya Mungu anayeishi na kuhesabika kuwa wana wa Mungu au wana wa Ufalme ulio juu(Ufalme wa Mbinguni) wa **Mungu Yehova**.
3. **Nguvu ya msalaba**-Imetupa mamlaka ya kumiliki,kutawala duniani pamoja na Yesu Kristo kwa kuwa tunatumia nafsi ya Yesu kama mdhamini wetu hapa duniani,**Luka 10:19.**

**4. Nguvu ya msalaba**-Imetupa utambulisho katika ulimwengu wa roho kuwa tunamilikiwa na Ufalme wa juu wa Mbinguni.**Tumepigwa mihuri katika paji zetu za uso kama ni mali ya Ufalme ulio juu**,shetani hana mamlaka juu yetu tumekuwa huru toka himaya na milki ya shetani.

**5. Nguvu ya msalaba** - Imetupa kibali cha unyakuo wa kanisa/kunyakuliwa.

**6. Nguvu ya Msalaba**-Imetupa Nuru,kupitia nafsi ya Yesu tumekuwa Nuru kama yeye alivyo Nuru hapa duniani .

Tumenunuliwa kwa gharama na thamani pale msalabani kwa Damu ya Yesu na Nguvu ya Msalaba.Msichafue mavazi yenu matakatifu mliyovishwa baada ya kuokoka maana nyinyi ni hekaru la Roho Mtakatifu mliyepewa kama ahadi baada ya kumpokea Yesu.Kabla hujaanza maombi omba sala ya toba ili unaposimama mbele za Mungu muwe wasafi ili mshtaki(Ibirisi)akose kosa la kuwashitaki na maombi yenu yakawe safi na manukato mbele za Mungu. Wale wote waliookoka,wanalindwa na nguvu za Mungu, wamezungukwa na moto uwakao (moto ulao), na Damu ya Yesu imewazunguka muda wote, Malaika watakatifu wanawalinda muda wote adui hawezi wafikia.Ulipookoka uliama nchi **(nchi au ufalme wa ulimwengu wa giza na kuamia nchi au ufalme wa ulimwenguwa Nuru).**

✞

# MAOMBI YA KUFUNGULIWA VIFUNGO NA MAGONJWA MBALIMBALI

## 1. KUVUNJA NA KUHARIBU MAAGANO NA MADHABAHU ZA UKOO JUU YAKO.

Baba katika jina la Yesu Kristo wa Nazareti aliye hai,navunja na kuharibu kila madhabahu iliyojengwa au ungamanishwa na mimi kupitia chochote changu au cha wanangu au cha ndugu zangu. Natumia jina lenye nguvu na uweza wote, jina lake Yesu Kristo kuvunja kila madhabahu za uovu zilizotushikilia. Najitenga nafsi yangu, roho yangu, maisha yangu yote na madhabahu yoyote ovu. Natuma Malaika Watakatifu mpite kila eneo walinzi wa kipepo waliotumwa kunilinda au timiza kusudi la madhabahu ovu, wakamateni, wafungeni pingu na kuwateketeza kwa moto kwa jina la Yesu. Natumia Damu ya Yesu, kufuta na kuvunja kila laana na maagano yaliyofanywa kwa kutamkwa na mababu na mabibi wa ukoo wangu Imeandikwa **Ufunuo wa Yohana 12:11;**

***"Nao wakamshinda kwa damu ya Mwana-Kondoo, na kwa neno la ushuhuda wao,ambao hawakupenda maisha yao hata kufa"***

Natumia Damu ya Yesu kuvunja na kufuta maagano yote maovu. Nateketeza kwa moto wa Roho Mtakatifu madhabahu zote na kufuta laana na mashtaka yote. Natumia Upanga ambao ni Neno la Mungu, nakata muunganiko kati yangu na madhabahu iyo na kujiweka huru. Natumia Damu ya Yesu nafuta jina langu katika kitabu cha agano ovu na naandika jina langu katika Kitabu cha uzima wa milele. Naruhusu Damu ya Yesu ipite mwilini mwangu,nafsini mwangu na kufuta kila laana, kila agano na kuachia umiliki wa Yesu Kristo ndani yangu.Natumia Damu ya Yesu kufanya agano jipya la Damu yake kuwa mimi ni wa Yesu na namilikiwa na Mungu anayeishi,tangu sasa si mali ya shetani. Ahsante Bwana Yesu kwa kuniokoa,kunisamehe,kuniweka huru na kufanya **Agano la Damu** yako nami **amina.**

## 2. MAOMBI YA KUWA HURU TOKA NGUVU ZA GIZA.

Kwa msaada wa nguvu ya utatu Mtakatifu wa Mungu yaani Mungu Baba, Mungu Mwana na Mungu Roho Mtakatifu ninajiachiria huru toka nguvu zote za giza zilizojiungamanisha nami katika ulimwengu wa roho.Kwa jina la Yesu navua kila vazi la kipepo, kishetani, kiganga, kichawi nililovishwa ili kuharibu maisha yangu. Natumia moto wa Roho Mtakatifu kuteketeza chochote cha ufalme wa giza hadi majivu kwa jina la Yesu.Ninajitenga na kila kizuizi kilichowekwa mbele yangu ili nishindwe fikia hatima yangu nzuri, natumia nyundo ambayo ni Neno la Mungu, navunja kila ukuta, mIlima na kila kizuizi kilichosimama mbele yangu kinachonizui.Nafuta kila alama, chapa, mihuri niliopewa katika ulimwengu wa roho inayonitambulisha kumilikiwa na shetani kwa Damu ya Yesu. Navunja kila maagano ya giza niliyounganishwa nayo kupitia nguo, chakula, ndoto kwa jina la Yesu. Naagiza jua la haki liangaze maisha yangu yote tangu sasa na kuruhusu moto wa Roho Mtakatifu kuteketeza kila mipango, michoro miovu toka kwa adui zangu wote kwa jina la Yesu Kristo wa Nazareti.

Natumia Damu ya Yesu,navunja kila madhabahu ovu, nasambaratisha kila kafara ovu iliyofanyika kinyume na maisha yangu. Nanyamazisha kila sauti ovu za kafara na kuruhusu Damu ya Yesu inene mema na uzima juu yangu. Nafuta kivuli changu na nafsi yangu katika madhabahu hizo na kujiweka huru tangu sasa. Nafungua uchumi wangu pia na kurudisha mali na fedha zangu zilizonyang'anywa na adui katika ulimwengu wa roho. Narudisha kila kilichoibiwa kama nyota,kibali,ndoa na kuvisafisha tena kwa Damu ya Yesu. Naruhusu nguvu ya Roho Mtakatifu inivuvie na kulinda maisha yangu yote na kuniacha huru toka nguvu za giza.Ahsante Bwana Yesu kwa kuniweka huru **amina** .

## 3. MAOMBI YA ULINZI WA ROHO MTAKATIFU.

Baba katika jina la Yesu Kristo aliye hai, ninaomba ulinzi wako mtakatifu, ulinzi wako mkuu na wenye nguvu kupitia Malaika zako watakatifu na Roho wako Mtakatifu.Imeandikwa katika Neno lako **Zaburi 91:11**

*"**Maana Mungu atawaamuru Malaika wake,wakulinde popote uendapo".***

Kwa jina la Yesu Kristo aliye hai ninaachia ulinzi wa Roho Mtakatifu katika safari yangu yote niishiyo hapa duniani, uchumi wangu, ndoa yangu, watoto wangu, shule yangu n.k. Roho Mtakatifu nakuruhusu ng'oa,haribu,bomoa, angamiza na uteketeze nguvu zote za giza zilizotumwa kuniharibia hatima na maisha yangu. Roho Mtakatifu futa kila mipango na michoro miovu iliyopangwa sirini kinyume na maisha yangu kwa jina la Yesu Kristo wa Nazareti. Naachia Moto wa Roho Mtakatifu uangamize na kuteketeza kambi zote za adui zilizojiinua kupigana nami, natuma moto wa Roho Mtakatifu uteketeze madhabahu zote ovu za adui kinyume nami hadi majivu pamoja na upanga wa Roho ambao ni Neno la Mungu ukachinje makuhani wote na roho zote chafu kwa jina la Yesu. Najifunika na Damu ya Yesu maisha yangu yote sasa na hata milele,Nawaruhusu Malaika wa Bwana mnilinde popote niendapo na niingiapo na Damu ya Yesu inifunike maisha yangu yote **Amina**.

## MAOMBI YA KUFANYA

## 4. AGANO LA DAMU YA YESU KWAKO

Katika jina lipitalo majina yote, jina la Yesu Kristo wa Nazareti , naifunika ndoa yangu kwa Damu ya Yesu.Ee Bwana Yesu, nakuita uikomboe ndoa yangu kutoka katika nguvu za giza. Kwa jina la Yesu ninaamuru kila mwakilishi wa giza alietumwa kufuatilia na kuharibu ndoa yangu aanguke chini na kufa kwa jina la Yesu. Natumia mamlaka ya Damu ya Yesu kufuta kila laana, mchoro na mipango miovu kinyume na ndoa yangu.

Nawafichua adui wote waliojificha na kuwafutilia mbali kwa jina la Yesu.Nakataa ndoa yangu haitavunjika, haitaharibika na wala roho ya mapooza haitaidhuru ndoa yangu kwa jina la Yesu. Nafuta kila hukumu na mashtaka yaliyosimamishwa kinyume na ndoa yangu kwa Damu ya Yesu.Roho Mtakatifu vunja, haribu, kila ukuta, kizuizi kilichowekwa mbele ya ndoa yangu kwa jina la Yesu. Nimechagua mimi na nyumba yangu yote kumtumikia Bwana Mungu anayeishi. Nafunga kila milango ya kiroho haitapitisha nguvu au roho yoyote toka kuzimu kinyume na ndoa yangu. Nafunika malangoyetu yote kwa Damu ya Yesu sasa na hata milele.Nazungusha ukuta wa moto na kuifunika ndoa yangu kwa Damu ya Yesu milele na milele. Karibu Bwana Yesu utawale maisha yetu, ndoa yetu, uchumi wetu tangu sasa na hata milele **amina.**

## 5. MAOMBI YA SHUKRANI

Baba uketiye mahali pa juu, nakuja mbele zako na shukrani zangu za dhati. Ahsante kwa uhai, pumzi, uzima na upendo ulionao kwangu kupitia Yesu Kristo kama mpatanishi wangu kwako. Ahsante kwa kunipigania na adui zangu na kunichagua kama mmoja wa wana wako wanaostahili kuuingia ufalme wako wa milele. Ahsante kwa ulinzi wa Malaika watakatifu wasiolala usiku na mchana wakinilindana adui zangu wote.Ahsante kwa kusamehe dhambi zangu zote nilizotenda toka kuzaliwa kwangu hadi sasa. Ahsante kwa kulinda uchumi wangu, ndoa yangu, kazi yangu na kuachiria neema yako juu yangu. Ahsante kwa kuniweka huru na nguvu za giza na kunipa kibali cha kuishi ufalme wa Nuru wa Yesu Kristo na wewe Mungu unayeishi – Mungu wa Israeli Mungu wangu ninayepaswa kukwabudu,kukutumikia na kukukimbilia. **Imba nyimbo tatu au nne za sifa unazozijua ili umalize maombi yako kwa sifa.**

Ahsante Bwana Yesu kwa upendo wako **amina.**

## UJUMBE WANGU KWAKO

Soma sana Neno la Mungu (Biblia), funga, Sali sana, tenda matendo mema, sikiliza mahubili ya Mungu anayeishi kwa watumishi wake wa kweli na utunze vazi lako la utakatifu.Nakutakiwa baraka nyingi na ushindi mkubwa katika safari yako ya wokovu .Kanisa la Bwana li karibu kunyakuliwa, unabii umetimia, usimwache Bwana Yesu ishi maisha ya utakatifu ili uwe mmojawapo katika wateule /watakatifu wanaotarajia kunyakuliwa.

***Iwapo umeguswa na huduma hii,unaweza kuchangia sadaka yako ili tuprint vitabu vingi na wengine wapokee uponyaji na kufikiwa na wokovu bure kama ulivyofikiwa wewe ili nao wauingia Ufalme wa Mbinguni na Bwana apate nyakua mavuno mengi siku ya unyakuo.*** Changia sadaka yako kwa namba hizi;

***Jina: Jesus Christ Ambassadors***
***M-Pesa: 0755734678( Waliopo Tanzania)***
***M-Pesa: +255755734678( Waliopo nje ya Tanzania)***
***Lipa kwa M- Pesa: 5495860***
***Lipa kwa Tigo pesa: 5660346***

Bwana akubariki sana,akuongezee ulipopunguza na akumbuke hazina yako ya Mbinguni **Amina.**

**MAHALI OFISI YA VITABU ILIPO:**

**Boko Magengeni** wilaya ya Kinondoni mkoa wa Dar-es-salaam upande wa kituo cha mabasi yanayoenda mjini.

**Mwandishi wa kitabu;**
**Petrida Karch**
**Email: petridakarch@gmail.com**
**+491758114293**